Taarifa inayopinga Ukeketaji wa Wanawake, kutoka kwa serikali ya Uskoti.

## UKEKETAJI NI NINI?

Ukeketaji inamaanisha ni utaratibu wowote ambao unatoa sehemu ndogo au sehemu yote kabisa ya sehemu za siri za mwanamke kwa sababu ambazo si za kimatibabu.

Ukeketaji pia unajulikana kama 'kukata' ama 'kutahiri' na wakati mwingine inatajwa kuwa 'sunna'. Hata hivyo, hakuna dini ambayo inaruhusu ukeketaji wa wanawake.

Ukeketaji ni zoezi la kitamaduni ambalo lina madhara mengi. Baadhi ya wasichana hufa kwa sababu ya kupoteza damu nyingi au maambukizi ambayo husababishwa na ukeketaji. Wanawake wanaweza pata shida za kiafya katika maisha yao yote na ukeketaji waweza sababisha ugumu kataka kujifungua. Hakuna faida za kiafya zinazotokana na ukeketaji.

## Sheria za Uingereza na USKOTI.

Ukeketaji ni hatia nchini Uskoti na katika Uingereza yote(1). Ni hatia kwa mtu yeyote kutekeleza, kusaidia au kupanga ukeketaji wa mtu mwingine hata ikiwa kitendo chenyewe cha kukeketa kitafanyika nje ya Uskoti.

*(1) Ni kinyume cha sheria, chini ya sheria ya Uskoti ya mwaka wa 2005 inayozuia ukeketaji nchini Uingereza, Welisi na kaskazini mwa Airishi, kitendo hicho ni hatia chini ya Sheria dhidi ya Ukeketaji.ya mwaka wa 2003.*

## ADHABU ZA UHALIFU.

Mtu yeyote atakayepatikana na hatia ya kosa la ukeketaji au la kusaidia na kuruhusu kosa kama hili atahukumiwa kifungo cha hadi miaka 14, faini au yote mbili.

## Msaada.

IIwapo upo nchini Uingereza na una shauku kuwa kitendo hiki kinaweza kutendekea au mtu unayemjua, zungumza na mwalimu, daktari, muuguzi wa shule, mhudumu katika jamii polisi au mtaalamu mwingine yeyote wa afya, elimu au mhudumu wa jamii na wataweza kukusaidia.

Unaweza pia kupiga simu kwa shirika la kuzuia ukatili kwa watoto (NSPCC) kwa nambari 0800 028 3550. Hii ni laini inayohudumu masaa 24 kwa wasichana na wanawake ambao wako katika hatari ya kukeketwa. Iwapo uko nchini Uingereza na upo katika hatari ya dharura au unahofia kuwa unaweza kusafirishwa nje ya nchi ili ufanyiwe ukeketaji, tafadhali wasiliana na polisi kwa kupiga 999.

Kama uko nje ya nchi na unahitaji usaidizi au ushauri, tafadhali piga simu kwa ofisi za kigeni za Jumuia ya Madola kwa nambari +44 (0) 20 7008 1500 au ofisi za Kamishna wa Uingereza au Ubalozi wa nchi unayoizuru.

## MAWASILIANO.

Kwa habari zaidi tembelea:
[www.fgmaware.org](www.fgmaware.org)
Au uwasiliane na mashirika yafuatayo:

**DIGNITY ALERT RESEARCH FORUM (DARF)**
Kukampeni na kuelimisha ili kumaliza ukeketaji.
dignityalert@hotmail.co.uk
www.darf.org.uk

**WOMEN'S SUPPORT PROJECT**

Habari na rasilimali kuhusu ukeketaji na habari za mashirika ya kusaidia.
0141 418 0748
wsproject@btconnect.com
www.womenssupportproject.co.uk/vawtraining/content/resources/234/

**SHAKTI WOMEN'S AID**
Msaada kwa wanawake na watoto wanaopitia unyanyasaji wakinyumbani au ndoa za lazima.
0131 475 2399
info@shaktiedinburgh.co.uk
www.shaktiedinburgh.co.uk

**AMINA: MUSLIM WOMEN'S HELPLINE**
Msaada na habari kwa wanawake kuhusu suala lolote.
0808 801 0301
info@mwrc.org.uk
www.mwrc.org.uk

Ujumbe huu unalenga kulinda wasichana kutokana na Ukeketaji.

Iweke ndani ya pasipoti yako au kibeti au mkoba ambao una ubeba wakitiwotehasaunaposafirinjeyanchi.Unaweza onyeshafamilia, marafiki,na jamaa yako Ujumbe huu unaweka wazi kuwa ukeketaji ni kosa kubwa nchini Uskoti na Uingereza Kote ikiwa na adhabu ya kiwango cha juu ya miaka 14 gerazani kwa mtu yeyote atakayepatikana na hatia ya kosa hilo.

Kauli hiiinaungwa mkono na Mawaziri wa Uskoti, Wakili Mkuu na Polisi wa Uskoti.

**Sahihi.**

| | |
|---|---|
| Mr Alex Neil<br>Cabinet Secretary for Social Justice Communities and Pensioners Rights | Ms Fiona McLeod<br>Minister for Children and Young People |
| Mr Michael Matheson<br>Cabinet Secretary for Justice | Mr Frank Mulholland QC<br>Lord Advocate |
| Ms Shona Robison<br>Cabinet Secretary for Health | Sir Stephen House QPM<br>Chief Constable, Police Scotland |
| Ms Angela Constance<br>Cabinet Secretary for Education and Lifelong Learning | |